


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa,
148 Br. ya Kayenze,
33383 Nyehunge,
SENGEREMA, MWANZA.

Unapojibu tafadhari taja:

Kumb. Na. AB.03/117/01/VOL.I/59/104

Tarehe 02 Mei ,2024

**TANGAZO LA NAFASI SITINI (60) YA KAZI YA MUDA WA MIEZI SITA YA WAKUSANYA
MAPATO (REVENUE COLLECTORS)**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buchosa anatangaza nafasi sitini (60) za kazi ya Mkataba ya wakusanyaji mapato (revenue collectors) ambao wataajiriwa kwa muda wa miezi sita kuanzia Tarehe 1, Julai hadi Tarehe 30, Desemba 2024 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mapato hayo yatakusanywa katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama vitakavyoonekana kwenye Mikataba itakayoandaliwa baada ya taratibu za ajira ya muda kukalimika.

MAJUKUMU YA KAZI:

1. Kukusanya mapato toka kwenye vyanzo vya mapato atakavyopangiwa.
2. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yaliyokusanywa kwa siku hiyo yanawekwa Benki.
3. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yanakusanywa kwa kutumia mashine ya kukusanyia mapato (POS MACHINE) na kutoa stakabadhi halali za Halmashauri.
4. Kuhakikisha kuwa mashine ya kukusanyia mapato (POS MACHINE) inakuwa katika hali nzuri na inatumika muda wote bila kuzimwa (inakuwa ONLINE).
5. Awe tayari kufanya kazi kituo chochote utakachopangiwa na msimamizi wa kazi.
6. Kufanya kazi yoyote utakayopangiwa na msimamizi wa kazi.

MALIPO

Malipo kwa kazi hii ni asilimia 5 (5%) ya makusanyo yatakayokusanywa na mkusanyo mapato katika chanzo husika kwa kila mwezi.


SIFA MUHIMU ZA WAOMBAJI:

1. Awe raia wa Tanzania ambaye ni mkazi wa Halmashauri ya Buchosa.
2. Awe amesajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania (TIN).
3. Awe na kitambulisho vya Taifa (NIDA).
4. Awe amehitimu kidato cha Nne au cha sita, aliyemaliza chuo itakuwa sifa ya nyongeza.
5. Awe na umri wa Miaka 18 hadi 45.
6. Awe na ujuzi wa kutumia kwa ufasaha simu janja (smart phone).
7. Mwombaji anatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika katika maeneo wanakotoka.
8. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha picha mbili (pass port size) za rangi za hivi karibuni.
9. Awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha Lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
10. Awe mwaminifu, mwadilifu, na mwenye weledi.
11. Awe hajawahi kupatikana na hatia kwa makosa ya jinai.
12. Mwombaji asiwe na deni lolote Halmashauri ya Buchosa katika mifumo yote miwili (TAUSI na LGRCIS) kwa wakusanya mapato waliowahi kufanya kazi na Halmashauri ya Buchosa.
13. Mwombaji atakayekidhi sifa zinazotakiwa ataajiriwa na kupangwa kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya mapato vya Halmashauri ya Buchosa.
14. Barua ya maombi ipitie kwa Mtendaji wa Kijiji au Kata.
15. Barua ya maombi iwe na namba za simu na anuani ya kuaminika.
16. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na viambatanisho vinavyohitajika kama vile nakala ya Cheti cha mlipa kodi (TIN) Cheti cha kidato cha nne au Kidato cha sita, NIDA Namba na zitumwe kwa Anwani ifuatayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,
HALMASHAURI YA BUCHOSA,
S.L.P 44,
BUCHOSA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe **16/05/2024** saa 9.30 Alasiri.

IMETOLEWA NA MKURUGENZI WA HALMSHAURI YA BUCHOSA


Benson P. Mihayo
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA**